

UTARATIBU WA UKATAJI WA LESENI ZA BIASHARA HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJJI

UTANGULIZI

Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji inaendelea kutoa Leseni za biashara kwa Mujibu wa sheria ya Leseni za Biashara ya Mwaka 1972 na marekebisho yake yote. Biashara zote zenye sura isiyo ya kitaifa au ya kimataifa inatolewa na Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji kwa viwango vya ada vilivyopo katika Jedwali la Ada za Leseni zinazopatikana katika Marekebisho ya Sheria ya Leseni za Biashara ya mwaka 2014 kifungu cha 8.

Ada za Leseni za biashara zimepangwa kwa aina ya biashara. Kila Biashara ina kiwango chake cha ada ya Leseni. Pia Ada za Leseni zimegawanyika katika maeneo ya kufanyia biashara kwa Mfano ada za Jiji na Manispaa, Ada za Makao makuu ya Halmashauri za Wilaya, Ada za miji midogo katika Halmashauri na Ada za Leseni za Vijijini.

VIGEZO /UTARATIBU WA UKATAJI WA LESENI

Ili mfanyabiashara aweze kupata Leseni yake ya Biashara anatakiwa kuwa na vigezo/nyaraka zifuatazo

1. Mteja anatakiwa kuwa na eneo la kufanyia biashara lisilo hamishika **“PREMISE”**
2. Mteja anatakiwa kujaza fomu ya maombi ya Leseni kwa usahihi na kupitisha fomu hiyo kwa mamlaka zinazohusika kama kifungu namba 14 katika fomu kinavyojieleza.
3. Mteja anatakiwa kuambatanisha cheti cha kuzaliwa/Kitambulisho kinachokubalika katika fomu ya maombi ya Leseni
4. Mteja anatakiwa kuambatisha kivuli cha cheti cha Mlipa kodi **“CERTIFICATE OF TIN NUMBER”**
5. Mteja anatakiwa kuambatisha cheti cha utakaso wa kodi **“ TAX CLEARANCE CERTIFICATE”**
6. Kwa biashara zilizosajiliwa kwa Jina la biashara ni lazima Cheti cha usajili na Extract from Register viambatanishwe.
7. Kwa biashara ya Kampuni mteja anatakiwa kuambatisha **“Memorandum of Understanding”** na Cheti cha Usajili.

KWA WAFANYABIASHARA WANAOHUISHA LESENI ZAO WANATAKIWA KUAMBATISHA NYARAKA ZIFUATAZO

1. Leseni iliyokwisha muda wake
2. Kuwasilisha Cheti cha utakaso wa kodi **“TAX CLEARANCE CERTIFICATE”**

HITIMISHO

Mara baada ya kukamilisha nyaraka zote taarifa za mteja zitaingizwa kwenye mfumo wa mapato wa Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji na kutengenezewa hati ya Madai **‘Payment Bill’**. Mteja atatakiwa kulipa ada ya Leseni Kupitia Benki ya NMB tawi la Kigoma, mara baada ya malipo mteja atakuwa amekamilisha taratibu zote na atapatiwa Leseni yake mara moja.

NB: Mteja akikamilisha taratibu zote atapewa Leseni yake ndani ya masaa 24.